

# Je, unajua kuhusu uchunguzi wa bila malipo wa saratani ya matiti?

Saratani ya matiti ndiyo saratani inayogunduliwa zaidi miongoni mwa wanawake.

Kama wewe ni mwanamke aliye na umri wa miaka 40 au zaidi, unastahili kufanyiwa uchunguzi wa bila malipo wa matiti wa mamogramu (Eksirei ya matiti) kwa kutumia BreastScreen SA kila baada ya miaka miwili.

Mamogramu ya uchunguzi kwa sasa ndio njia pekee iliyodhibitishwa ya kikliniki ya kugundua saratani ya matiti mapema, kabla ya dalili kuanza kujionyesha.

Kima cha kupona cha saratani ya matiti kinazidi kuboreshwa kila mwaka, lakini ugunduzi wa mapema wa saratani ya matiti ni muhimu sana kwa matibabu rahisi na yenye ufanisi zaidi.

Unafaa kuipa afya nzuri kipaumbele kwanza.

Miadi katika mojawapo ya kliniki zetu huchukua dakika 10 tu na wafanyakazi wetu wa kike pamoja na wataalamu wa radiografu watahakikisha kwamba unapitia katika hali tulivu iwezekanayo.

Ili kuweka miadi au kujua taarifa zaidi, tupigie simu katika 13 20 50. Huduma za bila malipo za mkalimani zinapatikana endapo utazihitaji.



# Hoja na Taarifa Muhimu

- > Saratani ya matiti ndiyo saratani inayogunduliwa zaidi miongoni mwa wanawake. Mwanamke 1 miongoni mwa 10 wanaoishi Australia Kusini watakuwa kuanza kuwa na saratani ya matiti kabla ya umri wa miaka 75.
- > Hatari ya kuanza kuwa na saratani ya matiti huongezeka kadri umri unavyoongezeka. 75% ya kesi za saratani ya matiti zinagunduliwa miongoni mwa wanawake waliona umri wa zaidi ya miaka 50.
- > Wanawake 9 miongoni mwa 10 waliogunduliwa na saratani ya matiti hawana historia yoyote ya familia ya ugonjwa huo.
- > Mamogramu za uchunguzi (Eksirei za matiti) kwa sasa ndio njia tu iliyo thibitishwa ya kugundua saratani ya matiti mapema, kabla ya mwanamke kugundua dalili zozote.
- > Huhitaji daktari kukupendekeza ili kuwa na miadi katika kliniki ya BreastScreen SA.
- > BreastScreen SA ina kliniki 7 na vitengo sogevu 3 ambavyo husafiri katika maeneo ya nchi kila baada ya miaka miwili.
- > Hata kama huwa unafanyiwa mamogramu za mara kwa mara ni muhimu kwako kuwa na “ufahamu wa matiti”. Chukuwa muda kugundua “mtazamo” wa kawaida na “hisi” matiti yako kwani hii itakusaidia kutambua mabadiliko yoyote ambayo yanaweza kutokea wakati wowote.
- > Muhimu: Kama utagundua mabadiliko yoyote kama vile dude jipya au hali ya kuwa na madude, mabadiliko katika ukubwa au umbo la matiti yako, usaha kutoka kwenye chuchu, maumivu au mabadiliko ya ngozi, weka miadi ili kujadili dalili hizi na daktari wako bila kuchelewa.
- > Habari njema ni kuwa viwango vya wanaopona saratani ya matiti vinaendelea kuboreshwa kila mwaka. Takwimu za hivi majuzi zinaonyesha kwamba wanawake waliogunduliwa na saratani ya matiti wanao uwezekano wa 89% ya kupona kama saratani yao itagunduliwa katika awamu za mapema.
- > Chukua hatua sasa ili kuweka miadi katika moja wapo ya kliniki zetu. Huduma zetu ni bila malipo na huduma za bure za ukalimani zinaweza kupatikana endapo utazihitaji.
- > Simu 13 20 50.